# MDHIHIRIKO WA FALSAFA YA KIAFRIKA KATIKA VITENDAWILI VYA KISWAHILI

***Adria Fuluge***

*Chuo Kikuu Mzumbe -Tanzania*
adriafuluge@yahoo.com

***Felista Juma Ngatungwa***
*Shule ya Sekondari Mtombozi- Tanzania*
Felistangatungwa@gmail.com

## Ikisiri

*Falsafa ya Kiafrika huweza kujidhihirisha kupitia vipengele mbalimbali vya maisha vinavyoakisi tajiriba za Waafrika wenyewe. Vipengele hivyo ndivyo vinavyoibua mitazamo mbalimbali ya kifalsafa inayojenga falsafa jumuifu ya Waafrika. Miongoni mwa vipengele hivyo ni vitendawili ambavyo huibua na kuipa jamii husika maarifa ya kifalsafa. Makala hii inafafanua baadhi ya vipengele vya falsafa ya Kiafrika vinavyodhihirika kupitia vitendawili vya Kiswahili. Inafanya hivyo ili kuonesha vipengele vya falsafa ya Kiafrika vinayopatikana katika fasihi simulizi ya Kiswahili, hususani katika vitendawili. Hii ni kutokana na sababu kuwa vitendawili vya Kiswahili vimebeba amali za kifalsafa, ambazo kwa kiasi kikubwa zinasaidia katika kuhifadhi maarifa ya kifalsafa ya jamii ya Waafrika kwa ujumla. Data za uchunguzi huu zilipatikana kwa njia ya udurusu wa matini mbalimbali, majadiliano ya vikundi na mahojiano uwandani. Aidha, Nadharia ya Sosholojia ya Kifasihi ndiyo iliyotuongoza katika kuchunguza falsafa ya Kiafrika inayopatikana katika vitendawili vya Kiswahili. Kwa ujumla, mtazamo wa nadharia hii unadai kuwa fasihi haiwezi kujitenga na jamii ambayo kwayo fasihi hiyo imechipuzwa na kukuzwa. Hivyo, nadharia hii imetuwezesha kuonesha jinsi falsafa ya Kiafrika ilivyobebwa na vitendawili vya Kiswahili. Kwa ujumla, makala imebainisha kuwa utanzu wa vitendawili una hazina kubwa katika kuhifadhi na kutunza maarifa ya falsafa ya Kiafrika, ambapo kupitia vitendawili hivyo, falsafa hizo zimedhihirika.*

## 1.0 Utangulizi

Dhana ya falsafa imejadiliwa na wataalamu mbalimbali kwa namna tofautitofauti. Wizara ya Elimu na Utamaduni (1992) inafafanua kuwa falsafa ni taaluma inayojishughulisha na kutafuta ukweli wa jambo kwa njia ya kutafakari. Wamitila (2010) anafafanua kuwa falsafa ni istilahi inayotumiwa kuelezea wazo au mawazo anayoyaamini mtu, mwandishi au mtunzi kuwa yale anayoyaandika, yana ukweli unaotawala misingi ya maisha. Kwa mtazamo wa mtaalamu huyu, falsafa ni imani na mawazo aliyonayo mtu juu ya jambo fulani kuwa ni kweli kulingana na maisha halisi ya jamii. Naye Fuluge (2021) anaeleza kuwa falsafa ni taaluma au mtazamo unaochunguza matumizi ya dhana, kupima hoja pamoja na mbinu za ujengaji hoja. Anaongeza kuwa falsafa hufanya uhakiki au tathmini na kuthibitisha au kutoa ushahidi wa hoja zinazozungumzwa na nadharia mbalimbali zinazohusu hali halisi ya maisha kwa kuzingatia imani, mila, desturi pamoja na mienendo aliyonayo binadamu. Kwa ujumla, maelezo ya wataalamu hawa yanatupa picha kuwa falsafa inaweza kufasiliwa kwa mitazamo miwili. Mosi, ni namna mtu anavyotafsiri ulimwengu na vitu vingine. Pili, falsafa inatazamwa kama taaluma inayochunguza dhana au kupima vitendo na mbinu za ujengaji hoja katika kuhitimisha mambo fulani. Hivyo, kwa mujibu wa makala hii, falsafa inachukuliwa kama taaluma au elimu ya kutafuta uhakika wa mambo fulani katika maisha kwa njia ya kuutafakari ulimwengu. Pia, inatazamwa kama taaluma inayojishughulisha na kudadisi hali halisi ya maisha ya binadamu katika jamii yake kwa kuzingatia imani, mila, desturi pamoja na mienendo aliyonayo binadamu. Mambo haya yote hujidhihirisha kupitia aina mbalimbali za falsafa kama vile Epistemolojia, Ontolojia, Mantiki, Itikeli, Kosmolojia, Ujumi na Eskatolojia.

Nayo falsafa ya Kiafrika kama inavyofafanuliwa na Faustine (2017) ni fikra au mitazamo mbalimbali inayoeleza masuala mahususi ya kimaisha, yanayohusiana na jamii ya Waafrika. Fikra au mitazamo hiyo ndiyo inayowawezesha kuutafakari ulimwengu wao kwa kuuhusisha na vitu vilivyomo, na hatimaye kuutilia maana. Kwa ujumla, falsafa ya Kiafrika

inaweza kuelezwa kuwa ni jumla ya fikra, mienendo, ukweli na matendo wanayoyaamini na kuyazingatia Waafrika katika nyanja mbalimbali za maisha yao.

Katika ulimwengu tunaoishi, kila jamii ina namna yake ya kuuelewa, kuuthamini na kuutathmini utamaduni wake. Matendo na kila akifanyacho mwanadamu akiamini kuwa ni kweli kulingana na matakwa ya jamii yake, ndiyo falsafa ya jamii hiyo. Aidha, kila jamii huishi kulingana na taratibu au miongozo inayokitwa ndani ya falsafa yake, ambayo huifanya jamii moja kutofautiana na nyingine. Kwa vile falsafa ya jamii fulani hujifungamanisha na maisha ya jamii hiyo, fasihi nayo kama sehemu ya jamii, hujinasibisha kwa namna ya moja kwa moja na falsafa ya jamii hiyo. Hii inatokana na sababu kuwa, fasihi ni zao la jamii na hutumika kama jukwaa la kuelezea uzoefu, kaida, mila na desturi za jamii husika. Pia, fasihi kama tawi mojawapo la sanaa, hutumika kudhihirisha falsafa ya jamii husika. Kwa maana hiyo, hatuwezi kuitenganisha au kuiondoa fasihi ya jamii husika katika kuchunguza falsafa ya jamii hiyo kwa sababu falsafa hubebwa na misingi ya vipera vya fasihi inayotawala na kutumika katika jamii hiyo. Kwa kutambua hilo, makala hii imeona ni vema kuchunguza mdhihiriko wa falsafa ya Kiafrika katika vitendawili vya Kiswahili kama kiwakilishi cha vipera vingine vya semi, ambavyo havikushughulikiwa na makala hii. Hii inatokana na ukweli kwamba falsafa ya Kiafrika hujidhihirisha pia katika vipera hivyo, lakini kutokana na ufinyu wa mawanda ya makala hii, haikuwa rahisi kuchunguza vyote kwa wakati mmoja.

## 2.0 Kiunzi cha Nadharia

Uchunguzi wa makala hii umeongozwa na Nadharia ya Sosholojia ya Kifasihi. Nadharia hii iliasisiwa na mtaalamu wa Kifaransa, Hippolyte Taine (1828-1893). Taine aliangalia kazi ya fasihi kama taswira ya kijiografia, kiutamaduni na kimazingira iliyochimbuka kutoka katika jamii husika. Akifafanua kuhusu nadharia hii, anasema kuwa kazi ya kifasihi inatakiwa kuchukuliwa kama taarifa ya kweli inayohusu maisha halisi ya watu. Kwa hiyo, nadharia hii inajishughulisha na kazi yoyote ya sanaa kulingana na hali ya jamii ambayo sanaa hiyo imechipuka na kukuzwa. Pia, hutumika

katika kuchunguza uhusiano uliopo baina ya kazi ya sanaa, jamii na namna jamii hiyo ilivyoundwa. Wananadharia wa sosholojia ya kifasihi wanazingatia mambo makuu mawili, ambayo ni: mosi, namna jamii inavyohusiana na fasihi na pili, namna fasihi inavyofanya kazi katika jamii.

Burke (1941) anaona kuwa kazi ya sanaa, ikiwa ni pamoja na fasihi, inatumia mbinu mbalimbali ambazo zinamsaidia mwanajamii kuelewa vizuri na kuongeza uwezo wa kujiongoza katika jamii yake. Wahakiki wa sosholojia ya fasihi wanaweka mkazo zaidi katika utendaji na msisitizo kuhusu dhima ya fasihi katika jamii. Wanaona kuwa fasihi ina dhima kubwa ambazo ni kuelimisha, kuburudisha na kuonya jamii.

Uchunguzi wa makala hii umejiegemeza zaidi katika mihimili miwili ya nadharia hii. Nayo ni, mosi, fasihi haiwezi kujitenga na jamii, ambayo kwayo imetengenezwa (Taine, 1873; Narizvi, 1982). Pili, kazi ya kifasihi ni taswira ya kijiografia, kimazingira na kiutamaduni, ambamo kwayo imechimbuka (Mungah, 1999). Mihimili hii imetusaidia kujadili namna falsafa ya Kiafrika inavyojitokeza katika vitendawili vya Kiswahili. Hii ni kwa sababu fasihi ya jamii fulani ina mfungamano na maisha ya jamii husika. Kwa hiyo, vitendawili vya Kiswahili vilivyotumika katika makala hii ambavyo vimesawiri falsafa ya Kiafrika, vimetokana na jamii na vinahusu maisha halisi ya jamii. Hivyo, vimetuwezesha kupata picha halisi ya maisha ya Waafrika na namna wanavyoishi katika mazingira yao halisi.

## 3.0 Methodolojia

Makala hii imejiegemeza katika utaamuli na siyo tarakimu kwa kuwa data zilizotumika zimechambuliwa na kuwasilishwa kwa njia ya maelezo katika kujenga maana ya maudhui yake. Njia za kukusanyia data zaidi ya moja zilitumika ili kuongeza uthabiti wa data za utafiti na kuondoa uwezekano wa kuwapo kwa hitilafu za kiutafiti kutoka kwa mtafiti au watafitiwa. Njia hizo ni udurusu wa maandiko, mahojiano na majadiliano ya vikundi lengwa. Udurusu wa maandiko ulifanyika ili kupata data zinazohusiana na vitendawili vya Kiswahili na namna vinavyosawiri falsafa ya Kiafrika. Pia, njia ya majadiliano ya vikundi lengwa kwa wanafunzi wa shule za msingi

na sekondari ilitumika kwa lengo la kupata vitendawili vya Kiswahili vinavyotumika katika jamii. Hivi vimesaidia kubaini namna falsafa ya Kiafrika inavyojitokeza katika vitendawili hivyo. Pia, kutumika kwa njia hii kulisaidia kuwapa uhuru watafitiwa wa kushiriki katika mjadala wakiwa na wanafunzi wenzao waliowazoea. Aidha, njia ya mahojiano ya ana kwa ana ilitumika na watoa taarifa walitoa data zinazojenga hoja kuwa falsafa ya Kiafrika, hudhihirika kupitia vipengele mbalimbali kama vile umoja na ushirikiano, uchawi na ushirikina, uhai na kifo, na uduara, vinavyojitokeza katika maisha ya mwanadamu ya kila siku.

## 4.0 Falsafa ya Kiafrika katika Vitendawili vya Kiswahili

Falsafa ya Kiafrika imekuwa ikisawiriwa katika tanzu mbalimbali za fasihi simulizi ya Kiafrika (Mbiti, 1969; Kezilahabi, 1985; Chuachua, 2016; na Mulokozi, 2017). Kama inavyosisitiza Nadharia ya Sosholojia ya Kifasihi, fasihi haiwezi kujitenga na jamii ambayo kwayo imechipuzwa. Hivyo, mambo mbalimbali yanayojitokeza katika jamii husawiriwa ndani yake. Hii ina maana kuwa fasihi inasawiri matendo ya jamii na kuonesha uhalisia wake kwa jamii. Uchunguzi wa makala hii umebaini kuwapo kwa falsafa mbalimbali zinazojitokeza katika vitendawili vya Kiswahili. Miongoni mwa falsafa zinazodhihirika katika vitendawili hivyo ni: umoja na ushirikiano, umuhimu wa maadili (ndugu wa damu), uhai na kifo, uduara, imani katika Mungu na mizimu, uchawi na ushirikina, na uzazi na malezi. Katika sehemu zinazofuata za makala hii tutachambua falsafa hizo kwa kina.

### 4.1 Falsafa ya Umoja na Ushirikiano

Suala la umoja na ushirikiano ni miongoni mwa mambo yanayozingatiwa katika jamii za Waafrika kwani wanaamini kuwa umoja na ushirikiano ni nguzo katika kufanikisha shughuli zao mbalimbali. Pia, wanaamini kwamba hakuna jambo linaloweza kufanyika vizuri pasipo kushirikiana na wengine (Mbiti, 1969; Kezilahabi, 1985; Oruka, 1990; na Samwel, 2015). Makala imebainisha kuwa mitazamo ya Waafrika imekitwa katika imani kuwa ushirikiano unajenga udugu ambapo katika umoja hakuna ubinafsi. Kwa hiyo, ushirikiano ndiyo nguzo ya kuimarisha mahusiano kuanzia katika ngazi ya kifamilia hadi ngazi ya jamii nzima. Falsafa ya umoja na

ushirikiano inadhihirika pia kupitia vitendawili mbalimbali vya Kiswahili. Katika mjadala wa vikundi lengwa, Godifrey[2] alitega kitendawili ambacho kinasawiri suala la umoja na ushirikiano kama ifuatavyo:

a) Kitendawili: Huyu kambeba huyu na huyu kambeba huyu na huyu kambeba huyu.
Jibu: Ardhi imebeba maji, maji yamebeba meli na meli imebeba watu.
**Chanzo**: Uwandani katika mjadala wa vikundi.

Katika kitendawili hiki, tumebaini kuwapo kwa falsafa ya Kiafrika inayosisitiza suala la umoja na ushirikiano. Aidha, kupitia kitendawili hiki imebainika kuwa kubebana huko kati ya ardhi, maji, meli na watu kunafanikisha masuala mbalimbali. Kwa mfano, bila kuwapo maji basi meli haitaweza kusafirisha watu na vitu. Hivyo, kitendawili hiki kinabeba falsafa ya umoja na ushirikiano kwa kuonesha jinsi masuala hayo yanavyorahisisha kazi, na hatimaye, kupata mafanikio yaliyokusudiwa.

Kitendawili kingine kinachosawiri falsafa ya umoja na ushirikiano ni hiki kifuatacho:

b) Kitendawili: Hufanya kazi daima wakiwa watatu.
Jibu: Mafiga.
**Chanzo**: Salla (2014)

Kitendawili hicho kinadhihirisha falsafa ya Kiafrika inayohusu umoja na ushirikiano. Akifafanua kuhusu kitendawili hiki, Rwiza[3] katika mahojiano yetu alieleza kuwa, "Waafrika wanaamini kwamba mtu hawezi kukamilika akiwa peke yake, bali ukamilifu wake unategemea kuwapo kwa watu wengine." Ufafanuzi wa mtaalamu huyu unatubainishia kuwa mitazamo ya

[2] Belina Godfrey ni mwanafunzi wa Shule ya Msingi Katerero iliyoko katika Halmashauri ya Wilaya ya Bukoba kata ya Kyeitema. Majadiliano yalifanyika tarehe 26.2.2020 shuleni hapo.

[3] Bw. Boniface Rwiza ni Mstaafu katika Utumishi wa Umma, Mwalimu wa dini na mtumishi wa kiroho wa Parokia ya Bikira Maria Mama Mwenye Heri Jimbo Kuu Katoliki la Bukoba. Mahojiano yalifanyika tarehe 4.3.2020 Kijiji cha Nyamkazi, Kata ya Kashai.

Waafrika kuhusu falsafa hii imekitwa katika imani kwamba ushirikiano ndiyo chachu ya kuyafikia maendeleo yanayotakiwa katika jamii.

Vilevile, mdhihiriko wa falsafa ya umoja na ushirikiano inajitokeza katika kitendawili kifuatacho:

c) Kitendawili: Kaa huku tukae kule tulenge mawe pangoni.
Jibu: Kula matonge ya ugali.
**Chanzo**: Badru (2015).

Kitendawili hiki kinasawiri suala la umoja na ushirikiano katika kufanya jambo. Dhana ya umoja inayobebwa katika kitendawili hiki inaonesha kuwapo kwa watu wawili au zaidi wanaotoa ushirikiano katika kufanya jambo fulani. Kokwenda[4] anashadadia jambo hili kama linavyojitokeza katika kitendawili hiki kwa kusema kuwa, “mkao wa kula wa watu waishio Bukoba ni ule unaotengeneza duara. Hii ni kwa sababu watu wanapokula hukaa katika uduara kuzunguka chakula kinachowekwa katikati.” Katika uduara huo, ndipo wanaweza kufahamishana na kujadiliana kuhusu mambo mbalimbali yanayotokea katika jamii na kuyapatia ufumbuzi. Mtazamo huu unatokana na imani za Waafrika katika ushirikiano kuwa ndio msingi wa mafanikio katika jamii. Hivyo, wanashirikiana katika kufanya mambo mbalimbali kwa pamoja na kula kwa pamoja.

Aidha, falsafa ya umoja na ushirikiano inajidhihirisha kupitia kitendawili kingine kama ifuatavyo:

d) Kitendawili: Nina bibi watatu, akiondoka mmoja wawili hawafanyi kazi.
Jibu: Mafiga.
**Chanzo**: Salla (2014).

[4] Bi. Olivia Kokwenda ni mwanajamii na mwalimu wa dini anayefundisha watoto katika Kigango cha Buyekera Jimbo Katoliki la Bukoba. Mahojiano yalifanyika tarehe 3.3.2020 Mtaa wa Buyekera, Kata ya Bakoba.

Uchunguzi umebaini kuwa kitendawili hicho kama ilivyo kwa vitendawili vilivyokwisha kujadiliwa, nacho kinaibua suala la umoja na ushirikiano. Matokeo yanaonesha kuwa maana ya kitendawili hiki imebeba dhana ya umoja na ushirikiano. Hii inatokana na sababu kuwa katika jamii ambazo hutumia mafiga kama nyenzo ya kupikia, kamwe haiwezekani kufanikisha zoezi hilo kama figa moja litaondolewa. Hii inaonesha kuwa bibi hawa watatu wanafanya kazi kwa pamoja na kila mmoja ana nafasi kwa mwingine. Kwa msingi huo, mmoja akitoka wawili wanaobaki hawawezi kufanya kazi wakiwa peke yao.

Akifafanua kuhusu falsafa hii kama inavyojitokeza katika kitendawili hicho, Rhenus[5] katika mjadala anadhihirisha mawazo haya anaposema:

> Katika maisha ya kila siku, Waafrika wana kawaida ya kushirikiana katika masuala mbalimbali. Huamini kuwa kila mtu ana nafasi yake kwa mwingine, hivyo, huishi kwa kutegemeana katika mambo mbalimbali. Jambo hili linadhihirika katika tanzu mbalimbali ambazo zinasawiri mawazo na utendaji wa Waafrika. Ni katika tanzu hizo kama vile vitendawili ambapo Waafrika huonya, hukosoa na huifunza jamii yao.

Maelezo hayo yanathibitisha suala la kutegemeana kwa Waafrika katika kufanya kazi mbalimbali kwa umoja kunakosaidia kuleta mafanikio. Hii ni kwa sababu umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu.

Hoja hii inaungwa mkono na Faustine (2019) anayeeleza kuwa suala la umoja na ushirikiano kwa Waafrika, ndio msingi wa kuimarisha na kudumisha mahusiano ya jamii kuanzia katika familia, ukoo hadi jamii nzima. Anasema:

[5]Amina Rhenus ni mwanafunzi wa kidato cha nne katika Shule ya Sekondari Kashai iliyopo Manispaa ya Bukoba, Kata ya Kashai. Majadiliano yalifanyika tarehe 25.2.2020 shuleni hapo.

> Mahusiano mazuri katika jamii za Waafrika yamesababisha kuwapo kwa umoja unaotazamwa kama kitambulisho kwa mgeni yeyote ajaye Afrika. Umoja na ushirikiano hufungamanishwa na sababu za kuwapo kwa mtu katika ukamilifu wa utu wake. Utu ambao umekitwa katika imani ya kuwapo kwa nguvu hai inayopatikana kutokana na namna mtu anavyoishi kwa kutii na kuzingatia mitazamo na maadili ya jamii yake. Hivyo, kwa Waafrika, ukamilifu wa mtu unatokana na au hutegemea uwepo wa watu wengine.

Kutokana na mawazo ya Faustine, tunaweza kusema kuwa, kwa Waafrika, mtu tajiri ni yule mwenye watu wengi kwani kuwapo kwao, kunamfanya kuwa mtu aliyekamilika. Kimsingi, Waafrika kwa kiasi kikubwa wanaishi kwa umoja na ushirikiano kulingana na mazingira yao kama inavyosawiri nadharia ya Sosholojia ya Kifasihi.

## 4.2 Falsafa ya Umuhimu wa Maadili katika Jamii

Maadili ni mwenendo unaokubalika ambao jamii imejiwekea kama msingi wa kuongoza jamii katika utaratibu unaofaa. Kila mtu, jamii au taifa, kwa jumla, huishi kulingana na maadili ya jamii hiyo (BAKITA, 2017). Makala imebainisha kuwa Waafrika ni miongoni mwa watu wanaoheshimu mila na desturi zao na huishi kwa kufuata miiko ya jamii hizo. Baadhi ya mila hizo ni kuheshimu wakubwa, kutoshiriki mahusiano ya kimapenzi na ndugu wa damu, na wizi. Waafrika wanaamini kuwa suala la maadili ni msingi katika kuyaendesha maisha yao; hivyo, maadili hayo yanajengwa kuanzia ngazi ya kifamilia, ukoo na hata jamii nzima. Aidha, mfumo wa maadili ya Waafrika unajengwa kidarajia kuanzia kwa mkubwa mpaka mdogo (Faustine, 2017). Kwa jumla, Waafrika wanaamini kuwa, maadili mema ni msingi wa kujenga amani, utu na adabu katika jamii. Falsafa ya Kiafrika kuhusu umuhimu wa maadili inathibitika kupitia tanzu mbalimbali vikimwamo vitendawili vya Kiswahili. Baadhi ya vitendawili hivyo ni:

a) Kitendawili: Miti yote nitakwea, mtarawanda utanishinda.
Jibu: Unaweza kumuoa yeyote lakini si ndugu wa damu.

**Chanzo**: Badru (2015, Jibu limerekebishwa).

Kitendawili hicho kinaonesha mtu mwenye uwezo wa kupanda miti yote isipokuwa mti wa mtarawanda. Swali linaloibuka akilini ni kwa nini ashindwe kupanda mti huo wakati mingine yote anaweza kuipanda? Je, huo ni mti wa namna gani? Maana ya kitendawili hiki ni kuwa, mtu anaweza kumuoa au kuolewa na mtu yeyote lakini si ndugu wa damu. Kitendawili hiki kinabeba falsafa ya Kiafrika inayokataza wanajamii kuwaoa ndugu zao wa damu. Falsafa hiyo inabainisha kuwa kuoana kwa ndugu wa damu kunaweza kusababisha laana, ambayo hupatilizwa na mizimu na wahenga wa ukoo husika.

Falsafa ya maadili inaendelea kujitokeza katika kitendawili kingine kama ifuatavyo:

b) Kitendawili: Nyumbani kwetu kuna papai lililoiva, lakini siwezi kulichuma.
Jibu: Mwali.
**Chanzo:** Badru (2015).

Kitendawili hiki kinaonesha taswira ya papai ambalo tayari limeiva lakini anayezungumza anasema kuwa hawezi kulichuma. Akielezea kuhusu kitendawili hiki, Dismas[6] katika majadaliano ya vikundi anafafanua kuwa:

> Taswira ya papai linalotajwa hapa inamaanisha binti au mwali ambaye tayari amefikia umri wa kuolewa lakini msemaji (kaka) anasema hawezi kulichuma (kumwoa au kuwa na uhusiano naye wa kimapenzi). Kwa hiyo, kitendawili hiki kinaibua suala la umuhimu wa kuzingatia maadili ya jamii za Waafrika yanayowakataza ndugu wa damu kuoana.

[6] Azas Dismas ni mwanafunzi wa kidato cha nne katika shule ya Sekondari Kashai iliyopo Manispaa ya Bukoba kata ya Kashai. Majadiliano yalifanyika tarehe 25.2. 2020 shuleni hapo.

Nukuu hiyo inaonesha kuwa falsafa hii ya maadili inayojitokeza katika kitendawili hicho, ndiyo inayomzuia kaka kumwoa dada yake, na hivyo, kutenda kinyume na katazo hilo ni kuvunja taratibu za jamii yenyewe.

Pia, kupitia mjadala, Josbert[7] alitega kitendawili kingine chenye maudhui sawa na haya kama ifuatavyo:

c) Kitendawili: Nina kitu kizuri sana nyumbani kwetu lakini siwezi kukichukua.
Jibu: Dada.
(**Chanzo**: Uwandani katika mjadala wa vikundi lengwa).

Kitendawili hiki pia, kinaibua maswali ya kujiuliza ni kwanini mzungumzaji anasema; ana kitu kizuri nyumbani kwao na asikichukue?. Ni kitu gani kinamzuia asikichukue?. Katika kujiuliza maswali hayo tunapata jawabu kuwa kitu kizuri hicho ni dada yake, ambaye ni mzuri sana lakini kwa kuwa yeye ni ndugu yake, hawezi kuwa na mahusiano ya kimapenzi wala kumwoa kwa sababu maadili hayaruhusu kufanya hivyo. Maelezo haya yanaungwa mkono na Rwekaza[8] anayefafanua kwamba:

> Siku zote watoto wa Kiafrika wamekuwa wakiishi kwa kuheshimu maadili hayo kuwa, dada au kaka, hata awe mzuri kiasi gani, haupaswi kumfikiria katika masuala ya kimapenzi; ni katazo katika jamii. Hii ni kwa sababu za kimaadili ya Kiafrika zinazokataza ndugu wa damu kuoana. Kwa kuwa, jamii inatambua kuwa inatakiwa kuishi katika maadili yanayofaa, ndiyo maana kitendawili hiki kinadhihirisha mawazo kuwa ndugu wa damu hawawezi kushiriki katika mahusiano ya kimapenzi.

Hivyo, kupitia mifano ya vitendawili hivyo kama vilivyofafanuliwa na watoa taarifa hao, tumebaini kuwa, jamii ya Waafrika ina maadili yake na mfumo wake wa kutolea na kujifunza mambo mbalimbali. Nadharia ya Sosholojia ya Kifasihi kupitia msingi wake unaosema kazi ya kifasihi ni taswira ya kijiografia, kimazingira, na kiutamaduni, ambamo, kwayo

[7] Jasintha Josbert ni mwanafunzi wa Shule ya Msingi Katerero iliyopo Halmashauri ya Wilaya ya Bukoba, Kata ya Kyeitema. Majadiliano yalifanyika tarehe 26.2.2020 shuleni hapo.
[8] Hashimu Rwekaza ni mwanajamii katika Wilaya ya Bukoba, Kata ya Hamugembe, Mtaa wa Nyangoye. Mahojiano yalifanyika tarehe 4.3.2020 nyumbani kwake.

imechimbuka ni uthibitisho kwamba Waafrika huishi kwa kuzingatia utamaduni wa jamii zao. Pia, huendelea kujifunza maadili kutokana na maisha yao ya kila siku kulingana na utamaduni husika.

## 4.3 Falsafa ya Uhai na Kifo

Falsafa ya uhai na kifo kwa Waafrika imeelezwa na wataalamu mbalimbali wakiwamo Tempels, 1959; Mbiti, 1969, Samwel, 2015; na Kaponda, 2018. Wataalamu hawa wanaeleza kuwa fikra kuhusu uhai na kifo ni masuala yanayowashughulisha sana Waafrika (Tempels 1959). Matokeo yanaonesha kwamba Waafrika huamini kuwa mtu akiumwa nguvu uhai hupungua, na huweza kupoteza uhai wake. Hii inatokana na kuamini kwao kwamba kifo ni matokeo ya laana inayotokana na kupungua kwa nguvu uhai (Fuluge, 2021). Imebainika kuwa, wakati mwingine, Waafrika huamini kwamba kifo husababishwa na mchawi. Data za uwandani zinathibitisha hoja hii kwani watoa taarifa walieleza kwamba kila mwanadamu atakufa ingawa siyo kila kifo kinachotokea ni mpango wa Mungu. Hii ni kwa sababu kuna vifo vingine vinasababishwa na wachawi. Mawazo haya yanathibitishwa na Abdallah[9] anayesema:

> Hatukatai kuwa ni kweli binadamu lazima afe lakini siyo kila kifo ni mpango wa Mungu. Mungu hakumuumba mwanadamu ili amwangamize lakini kuna watu wachache wasiopenda maendeleo ya watu wengine, ndio hutumia nafasi za nguvu zao kuwaangamiza kwa faida yao binafsi au kufanya visasi.

Maelezo hayo ni ithibati tosha kwamba Waafrika wana imani mbalimbali kuhusiana na masuala ya kifo.

Aidha, Kaponda (2018) anaeleza kuwa kwa Waafrika, kifo husababishwa na mchawi, roho za wafu, laana na kifo cha asili. Anaongeza kuwa mtu hufa taratibu mpaka watu wanaomkumbuka waishe. Anaendelea kufafanua kuwa

[9] Bi. Farida Abdallah ni mwanajamii na mwalimu mstaafu wa Shule ya Msingi ya Qudus iliyopo Manispaa ya Bukoba. Mahojiano yalifanyika tarehe 4.3.2020 mtaa wa *National Housing*- Kashai.

Waafrika wana hofu na kifo. Ithibati ya hoja hii ni kwamba katika msiba, watu huweza kulia na hata kuzimia pale wanapoondokewa na mtu waliyekuwa wanampenda na aliyekuwa na umuhimu kwao.

Aidha, falsafa ya uhai na kifo imebainika kupitia vitendawili vya Kiswahili vinavyotumika katika jamii za Kiafrika. Kitendawili kifuatacho ni mfano mmojawapo unaodhihirisha kuwapo kwa falsafa hiyo katika vitendawili vya Kiswahili:

a) Kitendawili: Ini la ng'ombe huliwa hata na walioko mbali.
Jibu: Kifo.
**(Chanzo**: Badru, 2015).

Watoa taarifa walifafanua kuwa Waafrika wanayo falsafa yao inayohusu masuala ya uhai na kifo. Akifafanua kuhusu suala la kifo kama linavyojitokeza katika kitendawili hiki, Katunzi[10] alieleza kuwa, "kifo humfika mtu yeyote na hakuna anayeweza kukikimbia ili aishi miaka yote hapa duniani. Walioko mbali hukumbwa na kifo na hata walioko karibu, nao hukumbwa na kifo." Maelezo hayo yanaendana na kitendawili husika kinachoonesha kuwa kifo kwa mwanadamu hakiepukiki. Kwa upande mwingine, mfano wa kitendawili hiki unaibua dhana ya ushirikiano wa Waafrika katika suala la kifo kwamba linawashughulisha hata walioko mbali. Hii ni kwa sababu wanaamini kuwa hili ni suala zito la kijamii na linatakiwa kupewa uzito fulani kwa kuzingatia kuwa kila mtu ataweza kukumbana nalo wakati wowote. Maelezo haya yanaungwa mkono na Badru (2015) anapofafanua kuwa "taarifa kuhusu msiba huwashughulisha sana Waafrika bila kujali umbali ambao kifo hicho kimetokea. Taarifa za kifo, hata kama kimetokea mbali, zinaweza kusambaa na kuwafikia hata walioko mbali." Haya yote yanathibitisha kuwa vitendawili vya Kiswahili hudhihirisha falsafa ya Kiafrika.

---

[10] Bi. Marina Katunzi ni mwanajamii wa Wilaya ya Bukoba na mtumishi katika taasisi ya *Wolrd Vision* tawi la Bukoba. Mahojiano yalifanyika tarehe 3.3.2020 ofisini kwake.

Falsafa ya Waafrika ya uhai na kifo inaendelea kujidhihirisha katika kitendawili kifuatacho:

b) Kitendawili: Akitokea watu wote hunung'unika na kuwa na huzuni.
Jibu: Ugonjwa au kifo.
**(Chanzo**: Salla, 2014).

Kitendawili hiki kinaonesha namna taarifa za ugonjwa au msiba zinavyoleta masikitiko na huzuni pale vinapotokea katika jamii. Hii ni kwa sababu kila mtu huogopa kufa, na hupatwa na huzuni anaposikia kwamba mtu fulani anaumwa. Hofu hiyo hutokana na imani kuwa mtu anapoumwa sana huweza kufa. Kitendawili kifuatacho kinachoshadidia mawazo haya kilitegwa na Gidius[11] katika mjadala:

c) Kitendawili: Kitanda changu cha dhahabu nikikilalia siamki tena.
Jibu: Jeneza.
**(Chanzo:** Uwandani kupitia mjadala wa vikundi lengwa).

Katika ufafanuzi wake kuhusiana na kitendawili hicho, Gidius anaeleza kuwa dhana ya kitanda hapa imechukuliwa kama jeneza ambalo msemaji anakiri kuwa akilalia hataamka tena. Maana inayotolewa katika kitendawili hiki inahusisha suala la kifo, ambapo mtu aliyefariki akishalazwa kwenye jeneza hataweza kuamka tena. Suala hili linaibua falsafa ya Waafrika kuhusu kifo na uhai kwani ni ukweli kwamba mtu akifa hawezi kurudi katika hali ya kawaida na kuwa nafsi hai.

Hivyo, tunaweza kuhitimisha hoja hii kwa kusema kuwa vitendawili hivyo pamoja na maelezo mbalimbali tuliyoyatoa, vinathibitisha kwamba masuala yahusuyo uhai na kifo ni mojawapo ya falsafa ya Kiafrika na kuwa Waafrika wana hofu na kifo.

[11] Nicera Gidius ni mwanfunzi wa kidato cha nne katika Shule ya Sekondari Kashai iliyopo Manispaa ya Bukoba, Kata ya Kashai. Majadiliano yalifanyika tarehe 25.2.2020 shuleni hapo.

## 4.4 Falsafa ya Uduara

Uduara ni mojawapo ya falsafa inayojitokeza katika jamii za Waafrika (Mbiti, 2010 & 2011; Samwel, 2015; na Duwe, 2016). Kwa mujibu wa Duwe (2016), kwa Waafrika, mtazamo kuhusu uduara hubainika kupitia matendo mbalimbali, hususani sanaa zao za maonesho. Matokeo ya yanaonesha kuwa Waafrika wanaamini kwamba vitu vizuri ni vile vilivyo katika umbo la duara. Aidha, imebainika kuwa falsafa ya uduara hujitokeza katika jamii nyingi za Waafrika kutokana na vitu wanavyotumia au mambo wanayoyafanya kuwa na umbo la duara. Vilevile, kupitia data za uwandani, imebainika kwamba jamii nyingi za Kiafrika hufanya mambo mbalimbali kama vile michezo ya watoto, mikao ya kula, shughuli za kijamii ikiwamo misibani na sherehe mbalimbali kwa uduara.

Katika makala hii, falsafa ya uduara imeweza kuthibitika pia kupitia vitendawili mbalimbali vya Kiswahili. Vitendawili hivyo vipo katika namna mbili. Mosi, ni vile vinavyoonesha dhana ya uduara katika vitu. Pili, ni vile vinavyoibua uduara katika utendekaji wa jambo. Kifuatacho ni kitendawili kimojawapo kinachoonesha utendekaji wa jambo katika uduara:

a) Kitendawili: Amekaa kimya na watoto wamemzunguka pande zote.
Jibu: Mgomba katikati na machipukizi yake pembeni yake.
(**Chanzo:** Salla, 2014).

Katika kukichunguza kitendawili tajwa, tumebaini kuwapo kwa falsafa ya uduara. Maana inayopatikana katika kitendawili hiki inaibua falsafa ya uduara kwa sababu Waafrika wanaamini kwamba kukaa kwa uduara kunasaidia kujenga mshikamano kuanzia katika familia, ukoo na jamii nzima. Akifafanua kuhusu kitendawili hiki, mtoa taarifa (hakutaka jina litajwe) katika mahojiano anasema:

> Uduara unajitokeza katika mambo mengi. Karibia kila jambo linalofanyika hufanywa kwa uduara. Kwa mfano, kwenye shughuli za kitanzia na sherehe mbalimbali za kijamii, mara nyingi matukio yake hufanyika kwa uduara. Hii inasaidia

hata kufahamiana kwa watu kwa kuwa wanakuwa wanaonana. Hapa inakuwa ni rahisi kutambua aliyeshiriki na yule ambaye hajashiriki katika shughuli husika ya kijamii. Kwa hiyo, utakuta wanapokula, wanapocheza au hata wanapozika huwa wanakuwa katika mzunguko unaotengeneza duara. Hii ndiyo maana kitendawili kinaonesha kuna kitu kilichopo katikati na wengine wamekizunguka pande zote kutengeneza duara.

Maelezo hayo ni ithibati kwamba kitendawili hicho kimesawiri vema falsafa ya uduara. Pia, kupitia mjadala wa vikundi lengwa, Clophas[12] alitega kitendawili kifuatacho kinachosawiri falsafa ya uduara:

b) Kitendawili: Askari wamekaa pembeni na mfalme yupo katikati.
Jibu: Watu wakiota moto huku wakiwa wameuzunguka.
(**Chanzo:** Uwandani katika mjadala wa vikundi lengwa).

Matokeo yanaonesha kuwa Waafrika huamini katika uduara na ndiyo maana, kwao mambo mazuri ni yale yaliyoko kwenye umbo la duara. Pia, imebainika kuwa kwa Waafrika, vitu vizuri ni vile vilivyoko katika umbo la duara. Kwa hiyo, kupitia falsafa hii hujikuta wakifanya mambo yao mengi wakiwa katika uduara.

Kitendawili kingine kinachodhihirisha kuwapo kwa falsafa ya Kiafrika katika vitendawili ni:

c) Kitendawili: Fupifupi la mviringo limeleta utamu.
Jibu: Ngoma.
(**Chanzo**: Salla, 2014).

Dhana ya uzuri katika kitu imejibainisha katika kitendawili hiki ambapo kichocheo chake cha msingi ni "fupifupi la mviringo kuleta utamu." Kupitia

[12] Eneliko Clophas ni mwanafunzi wa Shule ya Msingi Katerero iliyopo Halmashauri ya Wilaya ya Bukoba, Kata ya Kyeitema. Majadiliano yalifanyika tarehe 26.2.2020 shuleni hapo.

mfano huu, tumebaini kuwa falsafa ya Kiafrika inajidhihirisha kutokana na utamu unatokana na umviringo wa kitu hicho. Mawazo yaliyo katika kitendawili hicho yanafanana na ya Mlelwa (2017) anayesema:

> Utamaduni wa Waafrika unaonesha wazi kuwa wanaamini kitu chochote kikifanyika katika hali ya duara kinakuwa kizuri. Hii ni kwa sababu kunakuwa na umoja katika kutenda. Pia, kitu kikiwa katika umbo la duara kinakuwa ni kizuri. Kwa hiyo, umbo la duara ni kigezo cha uzuri kwa Waafrika.

Hoja hii inatiwa nguvu na Nadharia ya Sosholojia ya Kifasihi kupitia msingi wake unaosema, fasihi haiwezi kujitenga na jamii ambayo kwayo imechipuzwa. Hii ina maana kuwa fasihi inaakisi kile kinachotendeka na kukitoa kwa jamii. Matokeo yanaonesha kuwa vitendawili vinaakisi maisha halisi ya jamii kwa kusawiri falsafa yao.

### 4.5 Falsafa ya Imani katika Mungu na Mizimu

Wataalamu mbalimbali wanabainisha kuwa Waafrika huamini kwamba yupo Mungu ambaye ana uwezo wote (Tempels, 1959; Samwel, 2015, Chuachua, 2016, na Fuluge, 2021). Hii ni kwa sababu, Mungu anasawiriwa na kuelezwa na jamii mbalimbali duniani kote kuwa, ni mwanzo wa kuwapo na kuendelea kwa vitu vyote vinavyoonekana na visivyoonekana. Falsafa ya Kiafrika inadhihirisha kuwa jamii za Kibantu huamini kuhusu kuwapo kwa Mungu. Kwa mtazamo wa kiontolojia, Mungu anasawiriwa na kuelezwa na jamii mbalimbali duniani kote kuwa ni mwanzo wa kuwapo na kuendelea kwa vitu vyote vinavyoonekana na visivyoonekana (Chuachua, 2016; Fuluge, 2021). Pia, wataalamu hao wanakubaliana kuwa kuna mizimu ambayo ni daraja baina ya Mungu na wanadamu (Wiredu, 1980; Hountondji, 1983; Samwel, 2015). Aidha, wanaeleza kuwa Waafrika huamini kwamba mtu, na hasa aliye maarufu, anapokufa anabadilika na kuwa mzimu (Samwel, 2015). Falsafa kuhusu imani katika Mungu na mizimu inadhihirika katika vitendawili mbalimbali vya Kiswahili. Mifano ya vitendawili hivyo ni kama:

a) Kitendawili: Ana nguvu na uwezo kutushinda sote.
Jibu: Mungu.
(**Chanzo:** Salla, 2014).

Falsafa ya imani katika Mungu inajidhihirisha katika kitendawili hicho ambapo inaoneshwa kuwa Mungu ana uwezo wote na mkubwa kuliko wanadamu wote. Akifafanua kuhusu kitendawili hiki, Kigoye [13]katika mahojiano anasema:

> Kwa asili Mhaya anajua kuwa Mungu yupo ndiyo maana Mungu amepewa majina mengi kudhihirisha uwezo na nguvu zake. Baadhi ya majina hayo ni kama Ruanga[14], Katonda[15] na Nyarubamba[16]. Majina hayo yana maana tofautitofauti kudhihirisha uwezo na nguvu alizonazo Mungu.

Maelezo ya mtoa taarifa huyo yanadhihirisha kuwa kwa Waafrika, Mungu ndiye mtawala, asili ya kila kitu duniani na mwenye uwezo wa kutoa riziki kwa watu. Matokeo yanaonesha kuwa, licha ya imani kwamba Mungu ndiye muweza, bado Waafrika huamini katika wafu, yaani wahenga na mizimu ambayo huendelea kuwasikia wakiomba katika shida mbalimbali. Edisson[17] anashadadia kitendawili hiki kwa kusema:

> Mungu hashindwi na jambo lolote; akiamua lolote limtokee mwanadamu huwa linatokea. Jamii ya Waafrika inaamini kuwa, kuna viumbe vyenye nguvu na uwezo mkubwa wa

[13] Bw. Mwesigwa Kigoye ni mwanajamii na mtaalamu wa masuala ya mila za Wahaya wilayani Bukoba. Mahojiano na mtafitiwa yalifanyika tarehe 4.3.2020 mtaa wa Hamgembe Nyangoye.

[14] Ruanga ni jina la Mungu wa Kihaya linalomaanisha kuwa na uwezo wa kutoa maamuzi sahihi na anachokitolea maamuzi kinakuwa mwafaka.

[15] Katonda ni jina la Mungu lenye maana kuwa yeye ni asili ya kila kitu kilichopo duniani (muumbaji).

[16]Nyarubamba ni Mungu ana uwezo wa kila kitu hasa kwa upande wa kutoa riziki kwa watu.

[17] Happiness Edisson ni mwanafunzi wa Shule ya Msingi Katerero iliyopo Halmashauri ya Wilaya ya Bukoba. Majadiliano yalifanyika tarehe 26.2.2020 shuleni hapo.

> kutenda mambo ambayo binadamu wa kawaida hawezi kufanya. Viumbe hao ni kama vile Mungu, mizimu, wahenga na mababu. Ndiyo maana jibu la kitendawili chetu linaonesha ni Mungu tu ndiye mwenye uwezo huo.

Kitendawili kingine kinachodhihirisha falsafa ya Mungu na uwezo wake ni kile kilichotegwa na Selestine[18] kama ifuatavyo:

b) Kitendawili: Popote niendapo yupo lakini haonekani.
Jibu: Mungu.
**(Chanzo:** Uwandani katika mjadala wa vikundi lengwa).

Kitendawili hiki kinaonesha masuala ya imani ya Waafrika katika Mungu ambayo ndiyo kweli ya maisha yao. Akifafanua kuhusu kitendawili hiki, Selestine (ameshatajwa) anasema:

> Waafrika wanaamini kuwa, wapo viumbe wenye nguvu na uwezo wanaoaminika kuwapo lakini binadamu wa kawaida hawawezi kuwaona isipokuwa kupitia imani tu kuwa yupo. Pia, Waafrika huamini kuwa Mungu ana uwezo wa kutembea mahali popote na asiweze kuonekana kwa macho ya kawaida. Kwa hiyo kitendawili hiki kimesawiri vema falsafa ya imani katika Mungu na mizimu.

Aidha, hoja hii imetiliwa nguvu na Tempels (1959) kuwa Mwafrika anaamini kuna nguvu kubwa kuliko zote, yaani Mungu. Hivyo, ameamua kugawa nguvu hizo katika darajia za nguvu ambazo ni: Mungu > mizimu -> wahenga -> wazee -> binadamu wa kawaida -> wanyama -> miti. Kwa hiyo, kupitia maelezo ya mtaalamu huyu na nukuu ya hapo juu ni dhahiri kuwa Waafrika wanaamini katika nguvu za Mungu na mizimu katika kuwawezesha kufanikisha mambo mbalimbali. Hussein (1976) anakubaliana na hoja hii kwa mtazamo kuwa Waafrika wanaamini kwamba watu

[18] Faustine Selestine ni mwanafunzi wa kitato cha nne katika Shule ya Sekondari Kashai iliyopo Manispaa ya Bukoba. Majadiliano yalifanyika tarehe 25.2.2020 shuleni hapo.

waliokufa wapo karibu na Mungu na wale walio hai humwomba Mungu kupitia wale waliokufa. Hili linadhihirika kupitia matambiko au kuomba mizimu ya mababu inayofanywa na Waafrika wengi katika maisha yao ya kila siku. Hivyo, Waafrika wengi wanaamini kwamba wahenga wanaweza kuwa na nguvu katika kila kitu kinachowatokea katika maisha yao. Mambo kama vile kuumwa, vifo, ajali, talaka, mimba kuharibika, ulemavu na mikosi, inaaminiwa kutokea kwa sababu ya wachawi au hasira za mababu na wahenga. Kwa ujumla mawazo haya yanadhihirisha mtazamo wao kuhusu imani katika nguvu za Mungu na mizimu katika maisha yao halisi kama inavyoelezwa katika Nadharia ya Sosholojia ya Kifasihi.

### 4.6 Falsafa ya Uchawi na Ushirikina

BAKITA (2017) linaeleza kuwa uchawi ni ustadi wa kutumia kitu chochote kiushirikina kwa lengo la kumdhuru kiumbe mwingine. Naye, Makame (2016) anafafanua kuwa ushirikina ni tabia ya mtu kufanya matendo au maneno yaliyo juu ya uwezo mkubwa wa kiumbe kingine kuleta madhara badala ya ule wa Mwenyezi Mungu kwa kutumia majini, mizimu, talasimu za kisihiri na hirizi katika kufanikisha jambo fulani. Ushirikina hujitokeza katika nyanja mbalimbali ambazo ni mosi, kufanya matendo yasiyo ya kawaida ya kuogofya na kushangaza. Pili, mtendaji wa ushirikina hushiriki na kufuata maelekezo ya viumbe wa ajabu na kuwasiliana nao katika ufanikishaji wake. Tatu, mshirikina hutawaliwa na lugha za majini na mashetani pamoja na kuzungumza nao katika sehemu maalumu kama vile mapango au kilingeni. Makala imebainisha kuwa jamii nyingi za Kiafrika huamini katika nguvu za miujiza katika kutenda mambo yasiyo ya kawaida. Nguvu hizo hujulikana kuwa ni za kichawi au za kishirikina. Falsafa ya Kiafrika kuhusu uchawi na ushirikina inadhihirika katika kitendawili kifuatacho:

a) Kitendawili: Mchawi wa manga hulala mchana na kufanya kazi usiku.
   Jibu: Mwezi.
   **(Chanzo**: Salla, 2014).

Kitendawili hicho kinaonesha namna ambavyo wachawi hufanya kazi usiku. Hii inasawiri suala la imani za Waafrika kuhusu uchawi. Matokeo yanaonesha kuwa jamii nyingi za Kiafrika, huaminika kuwa ni za wachawi na hufanya shughuli za kichawi nyakati za usiku.

Pia, falsafa ya uchawi na ushirikina imedhihirika katika kitendawili kifuatacho:

b) Kitendawili: Kaa huku nikae kule tumfinye mchawi.
Jibu: Kula ugali kwa mikono.
**(Chanzo**: Badru, 2015).

Kitendawili hiki kinasawiri mapokeo ya jamii kuhusiana na uchawi. Akifafanua kuhusu kitendawili hiki, Theobard[19] katika mjadala anasema:

> Katika jamii za Kiafrika, japo uchawi upo, lakini bado haukubaliki miongoni mwa wanajamii na unapingwa vikali. Pindi wanapojua kuwa mtu wa jamii yao ni mchawi huweza kumkemea na kumdhihaki ili aachane na uchawi. Hivyo, maana ya kitendawili hiki inaibua dhana ya ushirikiano katika (kumfinya) kumwadhibu mchawi.

Maelezo haya yanaonesha kuwa Waafrika wanaamini katika masuala yanayohusu “uchawi na ushirikina” na wanawachukia wachawi na matendo yao. Katika kuunga mkono mtazamo wa hoja hii, Manala (2004) anasema:

> Wachawi siyo tu kwamba wanaogopwa lakini pia, wanachukiwa kwa sababu wanayafanya maisha bila shaka kuwa magumu kwa mtu binafsi, familia na hata jamii kwa jumla. Kwa mtazamo wa Waafrika, ikitokea magonjwa, bahati mbaya, ajali au hata vifo, basi watamtazama moja kwa moja mchawi kwamba ndiye aliyesababisha (Tafsiri ya waandishi wa makala).

[19] Adelaida Theobard ni mwanafunzi wa kidato cha nne katika Shule ya Sekondari Kashai iliyopo Manispaa ya Bukoba. Majadiliano yalifanyika tarehe 25.2.2020 shuleni hapo.

Nukuu hiyo inathibitisha kwamba, wachawi hawapendwi katika jamii na hupingwakwa sababu uchawi unahusisha matendo maovu. Faustine (2017) anaeleza kuwa Waafrika wanaamini mchawi anaweza kutumia viumbe wengine katika kutenda matendo mbalimbali kinyume na uhalisi wao au kumbadilisha mtu na kumfanya aishi katika ulimwengu wa wachawi bila watu wengine kumwona. Huko hutumikishwa na mchawi huyo kwa kufanyishwa kazi mbalimbali kama ilivyo katika ulimwengu wa kawaida.

Hivyo, tunaweza kuhitimisha hoja hii kwa kusema kwamba mtazamo wa Waafrika kuhusu falsafa ya uchawi, unajipambanua kwa kiasi kikubwa katika jamii za Kiafrika. Mawazo haya yanafungamanishwa na Nadharia ya Sosholojia ya Kifasihi inayosisitiza kuwa fasihi haiwezi kujitenga na jamii ambayo kwayo imechipuzwa. Hii ni kutokana na sababu kuwa kazi nyingi za fasihi ya Waafrika zimesawiri kwa wingi falsafa hii kama tulivyoona katika vitendawili tulivyovitumia katika hoja yetu, vinavyodhihirisha kuwapo kwa falsafa ya uchawi na ushirikina katika jamii ya Waafrika.

### 4.7 Falsafa ya Uzazi na Malezi

Suala la uzazi ni la muhimu sana kwa Waafrika. Matokeo yanaonesha kuwa Waafrika wanaamini kwamba ukamilifu wa ndoa za Waafrika unategemea uwezo wa mwanamke kuzaa watoto. Aidha, wanaamini katika familia pana ambapo kuzaa watoto wengi ni ufahari na kunaifanya familia au ukoo kupanuka. Fuluge (2021) anaunga mkono hoja hii kwamba Waafrika huthamini sana watoto. Anaongeza kuwa thamani ya mwanamke wa Kiafrika hupatikana kutokana na kuwa na uwezo wa kuzaa watoto wengi. Kulingana na Thatiah (2018), kutoweza kuwa na watoto huchukuliwa kuwa ni balaa na nuksi. Hii ni kwa sababu watoto huchukuliwa kuwa baraka katika ndoa na jamii kwa jumla. Naye Faustine (2017) anamwelezea mtu mwenye uzazi kutazamwa kama mtu mwenye baraka nyingi zinazotokana na kuwapo kwa nguvu-hai. Hii ni kwa sababu Waafrika wanautazama uzazi kama njia ya kuwapo kwa mtu na njia pekee ya kuukuza na kuuendeleza ukoo. Hivyo, mtu mwenye uzazi hupewa heshima kuliko yule asiye na uwezo wa kuzaa. Mbali na hilo, kupitia makala hii imebainika kwamba Waafrika wanaamini kuwa suala la malezi ya watoto hao ni jukumu la

wanawake kwa kiasi kikubwa. Hoja hii inaungwa mkono na Kayanga[20] aliyeeleza kuwa suala la uzazi na malezi ya watoto kwa Waafrika linamshughulisha mwanamke wa Kiafrika kuliko mwanamume.

> Suala la ndoa kwa jamii zetu linaenda sambamba na kuzaa kwa mwanamke. Mwanamke anapoolewa na kwenda ukweni anatarajiwa kumzalia mwanaume watoto. Mwanamke anayezaa hupendwa sana na wakwe zake ukilinganisha na yule asiyezaa. Siku zote mwanamke aliyeolewa na asizae hudharauliwa na hata kusemwa na ndugu wa mwanamume kwa kuwa hajaileteа faida familia au ukoo wao.

Maelezo hayo ni ithibati kuwa wanawake wa Kiafrika ndio wanaobebeshwa mzigo wa malezi ya watoto na pindi familia inapokosa uzazi mwanamke ndiye hupewa lawama zote. Maelezo haya yanaungwa mkono na De Beavoir (1985) kama alivyonukuliwa na Fuluge (2021) anapoeleza kwamba asasi ya ndoa inampa mwanamke majukumu mawili muhimu, ambayo ni: kuzaa watoto na kuhakikisha kuwa anamtimizia mume wake mahitaji ya kimapenzi, pamoja na kuangalia nyumba yake. Falsafa hii ya uzazi inadhihirika katika vitendawili mbalimbali vya Kiswahili. Theobard[21] alitega kitendawili kinachosawiri falsafa ya uzazi kama ifuatavyo:

a) Kitendawili: Dada yangu hazai mtoto mmojammoja, bali mapacha wengi wakubwa kwa wadogo.
Jibu: Mapapai.
**(Chanzo**: Uwandani katika mjadala wa vikundi lengwa).

Katika kitendawili hiki tumebaini kuwapo kwa falsafa ya Kiafrika ambayo imejikita kwenye uzazi. Hapa tunaiona falsafa ya uzazi ambayo inasisitiza umuhimu wa kuzaa watoto wengi. Kama mti wa mpapai unavyozaa matunda mengi ndivyo unavyofananishwa na uzazi wa watoto kwa

[20] Bi. Salma Kayanga ni mwanajamii, mama wa familia na Afisa afya ofisi ya Kata ya Kibeta. Mahojiano yalifanyika tarehe 5.3.2020 ofisini kwake.

[21] Teodata Teobard ni mwanafunzi wa darasa la saba katika Shule ya Msingi Katerero iliyopa Halmashauri ya Wilaya ya Bukoba. Majadiliano yalifanyika tarehe 26.2.2020 shuleni hapo.

Mwafrika. Matokeo yanaonesha kwamba familia yenye watoto wengi huwa imara na thabiti katika nyanja mbalimbali.

Mfano mwingine wa kitendawili chenye falsafa ya malezi ni:

b) Kitendawili: Mama yangu kila aendako na mtoto wake mgongoni.
Jibu: Konokono.
(**Chanzo**: Salla 2014).

Matokeo yanaonesha kwamba kitendawili hiki kinasawiri suala la uzazi na malezi. Hii ni kwa sababu kinamtaja mama na mtoto wake mgongoni. Pia, kinaeleza kuwa mama huyu kila anakokwenda anakuwa na mtoto wake na katu hamwachi. Aidha, kinaibua suala la mahusiano ya mama na mtoto katika mazingira halisi ya maisha ya jamii kama inavyosisitiza Nadharia ya Sosholojia ya Kifasihi. Mahusiano hayo yanadhihirika katika jamii zetu kwani mama wa Kiafrika ndiye anayeonekana kuwajali sana watoto wake kila wakati ikilinganishwa na akina baba.

Falsafa ya uzazi na malezi inaendelea kudhihirika katika kitendawili kingine kama ifuatavyo:

c) Kitendawili: Wakikua mama yao huwatupa nje kwa kishindo.
Jibu: Mbaazi au mnyonyo.
**(Chanzo**: Badru, 2015).

Katika kukichunguza kitendawili hiki tumebaini kuwapo kwa falsafa ya Kiafrika juu ya uzazi na malezi. Falsafa hii inasisitiza kuwa watoto wanapaswa kupewa malezi bora hadi wafikie umri wa kuweza kujitegemea. Hii ina maana kuwa wakiwa katika umri mdogo kabla ya kuanza kujitegemea, wanakuwa katika uangalizi wa mama mpaka pale watakapokuwa wakubwa na kuweza kujitegemea.

Aidha, tumebaini namna kitendawili hiki kinavyosawiri falsafa ya malezi kwamba watoto hao, tangu wakiwa wadogo, wanakuwa katika mikono ya malezi ya mama zao. Falsafa hii inasisitiza umuhimu wa jamii kuwa na

watoto wenye malezi bora. Aidha, kupitia Nadharia ya Sosholojia ya Kifasihi katika msingi wake unaosisitiza kuwa fasihi haiwezi kujitenga na jamii ambayo kwayo imechipuzwa; tumeweza kuthibitisha kuwa falsafa ya Kiafrika haitoki katika ombwe, bali hutoka katika jamii husika. Hii ni kwa sababu vitendawili tulivyovitumia katika hoja yetu vimedhihirisha suala la malezi ya watoto katika jamii za Kiafrika kuwa ni jukumu la mama zaidi kuliko baba. Kwa hiyo, vitendawili hivi ni mali ya jamii kwani yanayozungumzwa ndani yake yanahusu jamii husika.

## 5.0 Hitimisho

Makala hii ilikusudia kuchunguza mdhihiriko wa falsafa ya Kiafrika kama inavyojitokeza katika vitendawili vya Kiswahili. Makala ilijikita katika kufafanua falsafa yenyewe kwa kuonesha imani na mitazamo ya Waafrika kuhusiana na falsafa husika huku ikithibitisha kwa mifano mbalimbali ya vitendawili vya Kiswahili. Miongoni mwa falsafa zilizojadiliwa ni falsafa kuhusu umoja na ushirikiano, uchawi na ushirikina, uzazi na malezi, uduara, kifo na uhai, maadili katika jamii, na imani katika nguvu za Mungu na mizimu. Aidha, utanzu wa vitendawili umedhihirika kuwa na hazina kubwa katika kuhifadhi na kutunza maarifa ya falsafa ya Kiafrika kama ilivyodhihirika katika makala hii.

## Marejeleo

Badru, Z. A. (2015). Taswira na Ubainishaji wa Mabadiliko ya Kiujumi katika Vitendawili: Mfano wa Vitendawili vya Kiswahili. Tasnifu ya Shahada ya Uzamivu katika Fasihi ya Kiswahili (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dodoma.

BAKITA, (2017). *Kamusi Kuu ya Kiswahili ya BAKITA*. Dar es Salaam: Longhorn Publishers Ltd.

Burke, K. (1941). *The Philosophy of Literary Form: Studies in Symbolic Action.* Baton Rouge, Louisiana: Louisiana State University Press.

Chuachua, R. (2016). Falsafa ya Riwaya za Saaban Robert na Euphrase Kezilahabi katika Muktadha wa Epistemolojia ya Kibantu. Tasnifu ya Shahada ya Uzamivu katika Fasihi ya Kiswahili (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dodoma.

Duwe, M. (2016). Mdhihiriko wa Falsafa ya Uduara katika Sanaa za Maonyesho za Jamii ya Wangoni. Tasnifu ya Uzamili katika Fasihi ya Kiswahili (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dodoma.

Faustine, S. (2017). Falsafa ya Waafrika na Mtindo wa Uhalisiajabu katika Riwaya ya Kiswahili. Tasnifu ya Shahada ya Uzamivu katika Fasihi ya Kiswahili (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dodoma.

Faustine, S. (2019). Falsafa ya Waafrika kama Kijenzi cha Mtindo wa Uhalisiajabu katika Riwaya za Kiswahili. Katika Ponera, A. S & Badru, Z. A (Wah), *Koja la Taaluma za Insia*: *Kwa Heshima ya Profesa Joshua S. Madumulla*. Dar es Salaam: Karljamer Publishers Ltd.

Fuluge, A. (2021). Usawiri wa Mchakato wa Kujiua katika Riwaya za Euphrase Kezilahabi: Ni Mwangwi wa Mtanziko wa Kijamii? Tasnifu ya Shahada ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dodoma.

Hountondji, P. J. (1983). *African Philosophy: Myth and Reality*. (Mfasiri: Henri Evans akishirikiana na Jonathan Lee). Bloomington: Indiana University Press.

Hussein, E. (1976). *Kinjekitile*. Nairobi: Oxford University Press.

Kaponda, G. J. (2018). Ontolojia ya Kiafrika katika Mbolezi za Wanyasa. Tasnifu ya Shahada ya Umahiri katika fasihi ya Kiswahili (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dodoma.

Kezilahabi, E. (1985). African Philosophy and the Problem of Literary Interpretation. Tasnifu ya Shahada ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Wisconsin Madison.

Mbiti, J. S. (1969). *African Religion and Philosophy*. London: Morrison and Gibb Ltd.

Mbiti, J. S. (2010). *Introduction to African Religion*. Kampala: East African Educational Publishers Ltd.

Mbiti, J. S. (2011). *African Religions and Philosophy*. Kampala: East African Educational Publishers Ltd.

Makame, S. F. (2016). Matumizi ya Falsafa ya Usihiri katika Riwaya Teule za Euphrase Kezilahabi. Tasnifu ya Shahada ya Uzamili katika Fasihi ya Kiswahili (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dodoma.

Manala, J. M. (2004). Witchcrafts and its Impact on Black African Christians*: A Lacuna in the Ministry of Hervormde Kerk in Suidelike Africa*. University of South Africa. Katika http://www.researchgate.net/publication/45681425. Ilisomwa tarehe 28.9.2020.

Mlelwa, A. A. (2017). Falsafa ya Kiafrika katika Vitabu Teule vya Fasihi ya Kiswahili: *Dunia Uwanja wa Fujo* na *Ngoma ya Ng'wanamalundi*. Tasnifu ya Shahada ya Umahiri katika Fasihi ya Kiswahili (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dodoma.

Mulokozi, M. M. (2017). *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili*. Dar es Salaam: KAUTTU.

Mungah, C. I. (1999). Dhana ya Maisha katika Novela Mbili za Kezilahabi: *Nagona* na *Mzingile*. Tasnifu ya Shahada ya Umahiri katika Fasihi. (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Nairobi.

Narizvi, S. (1982). *The Sociology of Literature of Politics*. Australia: Edamund Burke.

Oruka, H. O. (1990). *Trends in Contemporary African Philosophy*. Nairobi: Nairobi Publishers.

Salla, H. D. (2014). *Vitendawili vya Kikwetu*. Dar es Salaam: African Proper Education Network.

Samwel, M. (2015). *Umahiri katika Fasihi ya Kiswahili*: *Mwongozo kwa Mwanafunzi na Mwalimu wa Faasihi Simulizi na Andishi*. Dar es Salaam: Meveli Publishers (MVP).

Taine, H. (1873). *The Philosophy of Art*. New York: Holt & Williams.

Tempels, P. (1959*). Bantu Philosophy*. Paris: Presence Africaine.

Wamitila, K. W. (2010*). Kanzi ya Fasihi: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi: Vide Muwa Publishers.

Wiredu, K. (1980). *Philosophy and African Culture*. London: Cambridge University Press

Wizara ya Elimu na Utamaduni. (1992). *Historia ya Falsafa ya Elimu*. Dar es Salaam: National Printing Company.